# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
## WIZARA YA KILIMO
## WAKALA WA TAIFA WA HIFADHI YA CHAKULA
Kizota Viwandani Area | S.L.P 1050 Dodoma | Simu: +255(0)26 2963953 | Fax:+255(0)26 2963950
Barua pepe: info@nfra.go.tz | Tovuti: www.nfra.go.tz


## TANGAZO KWA UMMA

## KUHUSU UUZAJI WA MAHINDI MEUPE

Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula (NFRA) ni Wakala wa Serikali chini ya Wizara ya Kilimo ulioanzishwa kwa sheria ya Wakala za **Serikali Sura Na. 30 ya** mwaka 1997 kwa madhumuni ya kuhakikisha usalama wa chakula nchini. Katika kutekeleza moja ya majukumu yake, Wakala huzungusha akiba ya chakula (recycling) kwa kuuza nafaka zilizohifadhiwa ghalani ili kupata nafasi ya kuhifadhi nafaka zingine.

Wakala unatarajia kuuza **tani 33,489.447** za mahindi meupe**.** Mahindi hayo yatauzwa kupitia kanda zifuatazo za Wakala:-

| NA. | KANDA | KITUO | KIASI KITAKACHOUZWA (TANI) |
|---|---|---|---|
| 1 | Arusha | Themi | 641.842 |
| 2 | Dodoma | Kizota - Dodoma | 1,295.733 |
| | | Manyoni - Singida | 344.392 |
| 3 | Kipawa | Chang'ombe - Dar es salaam | 393.405 |
| 4 | Makambako | Makambako | 10,427.177 |
| 5 | Songwe | Mbozi - Vwawa | 577.432 |
| 6 | Shinyanga | Shinyanga- (Shinyanga Municipal) | 4,108.813 |
| 7 | Songea | Ruhuwiko - (Songea Municipal) | 4,003.546 |
| 8 | Sumbawanga | Mazwi - (Sumbawanga Municipal) | 9,008.087 |
| | | Laela - (Sumbawanga Rural) | 2,689.020 |
| | **JUMLA** | | **33,489.447** |

i) Mahindi yatauzwa kama yalivyo katika maghala ya Wakala (Ex-Warehouse) yakiwa yamefungashwa kwenye magunia.

ii) Mnunuzi atalipa gharama za ununuzi wa mahindi ndani ya siku 5 za kazi baada ya kupewa idhini ya kufanya malipo na kuchukua mahindi yaliyolipiwa ndani ya muda atakaopangiwa wa kuzingatia kiasi cha mahindi kilicholipiwa.

iii) Mnunuzi atalipia gharama zote za ubebaji na usafirishaji wa mahindi hayo.

iv) Mnunuzi ataonesha bei ya kununulia kwenye barua yake ya maombi pamoja na ghala la kuchukulia.

v) Wakala utapitia, kuchambua na kufanya maamuzi ya bei kwa kuzingatia bei iliyoombwa, bei ya soko, gharama zingine na kituo husika cha mauzo.

Hivyo Wakala unakaribisha maombi kutoka Taasisi mbalimbali, wasagishaji, watu binafsi, wafanyabiashara na wadau wa nafaka ili kununua mahindi. Maombi yabainishe bei ya kununulia, kiasi cha mahindi kinachohitajika, ghala la kununulia, anwani ya mwombaji pamoja na mawasiliano ya simu/barua pepe.

Wale wote waliokwisha wasilisha maombi yao katika Ofisi za Wakala kabla ya tangazo hili wanatakiwa kuwasilisha maombi mapya kwa kuzingatia maeneo ya mauzo. Maombi yanatakiwa kuufikia Wakala kabla ya **tarehe 06 Januari, 2021**. Kwa taarifa zaidi mnunuzi anaweza kuwasiliana na Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula kupitia **Simu namba 026 2963953**.

Maombi yatumwe kwa:

**Afisa Mtendaji Mkuu,**
Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula,
Kizota, Eneo La Viwanda,
S.L.P 1050,
**DODOMA.**
Barua pepe:- **info@nfra.go.tz**

Imetolewa na:

**Afisa Mtendaji Mkuu,**
**Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula**